Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Tanzania

(Agricultural Sector Development Programme - ASDP)

# Jarida la ASDP

Juzuu II Na. 3&4 (Julai-Desemba 2005)

**Kutoka kwa Mhariri:**

Waandishi Katika toleo hili, wameelezea juu ya maendeleo ya uanzishwaji wa Mfuko wa pamoja wa Kugharamia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo; Kutekeleza programu kwa kuzingatia Mtazamo Mpana wa Sekta katika kuendeleza sekta ya kilimo Tanzania; Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani; na maendeleo ya Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani.

Kuanzishwa kwa mfuko wa pamoja wa Programu ni hatua ya awali katika kuelekea kwenye kuimarisha Bajeti kuu ya Serikali ambapo serikali na wafadhili wameshirikiana kuandaa Programu na kukubaliana kusaidia kuiendeleza sekta ya kilimo kwa kufuata taratibu za kuwa na mfuko wa ASDP ambazo baadaye zinajumuishwa kwenye Muundo wa Muda wa Kati wa Matumizi ya serikali.

Uanzishwaji wa mfuko huo unasababisha kuwepo kwa umuhimu wa kuanzishwa kwa Mtazamo Mpana wa Sekta , licha ya mapungufu kadhaa yaliyoainishwa katika jarida hili. Kupitia hatua hizi, wizara kadhaa, hususan Wizara kuu za Sekta ya Kilimo zikiwemo Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya mifugo, Wizara ya Ushirika na Masoko na Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wafadhili watawekeza kwa pamoja na kuratibu rasilimali ili kukuza sekta hiyo.

Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo utakaoshirikisha wilaya 25 za mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga utazinduliwa rasmi mwezi Januari 2006, unalenga kuweka misingi bora ya uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Uendelezaji wa Kilimo Vijijini kwa kuunda na kuimarisha uwezo wa vikundi na mitandao ya wakulima. ***Sekretariati ya ASDP inawatakia mwaka wa mafanikio wa 2006***

## Yaliyomo

Maoni ya Mhariri 1

Mfuko wa pamoja wa kugharamia programu ya Sekta ya kilimo : Ni mpito wa kuelekea kwenye Bajeti kuu ya serikali 1

Mwelekeo wa Mtazamo Mpana wa Sekta katika Kuendeleza Kilimo 2

Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani 3

Maendeleo ya Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani 4

Kamati Maalum ya II ya Kushauri Programu Yazinduliwa 4

**Matukio Mengine ya Programu**

- Serikali na Wafadhili Kutathmini Mfuko wa pamoja wa kugharamia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, Januari, 2006
- Uanzishaji Shughuli zinazogharamiwa na mfuko wa pamoja wa Programu, Januari, 2006
- Kuzinduliwa Rasmi kwa Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo—16 Januari 2006.

## Mfuko wa Pamoja wa Kugharamia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo: Mpito wa Kuelekea kwenye Kuimarisha Bajeti Kuu ya Serikali

Lengo la kuimarisha Bajeti Kuu ni kuipa serikali uhakika wa rasilimali za uwekezaji ili kupanga na kutumia fedha za bajeti kulingana na vipaumbele vya maendeleo.

Bajeti ya serikali iliyoimarishwa itachangia katika lengo kuu la kupunguza umaskini chini ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini ( MKUKUTA).

Mkakati wa kuunganisha Misaada ya Wafadhili unaainisha ubora wa kugharamia maendeleo kwa kupitia bajeti kuu iliyoimarishwa lakini unaruhusu njia zingine za kugharamia maendeleo katika kipindi cha mpito.

Uandaaji wa Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo umejikita katika Mtazamo Mpana wa Sekta katika kutatua matatizo yake na hautegemei taratibu zitakazotumika kugharamia programu.

Mfuko wa pamoja wa kugharamia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ni sehemu ya uimarishaji wa bajeti kuu ya serikali kwa sababu zifuatazo:

- Sifa ya kipekee ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ni namna ilivyo na mtazamo wa kitaasisi kwenye kukabialiana na umaskini, eneo ambalo ni muhimu katika kujenga uwezo wa serikali za mitaa katika kusimamia maendeleo kwa kupitia mipango ya maendeleo ya kilimo wilayani; na kuwezesha serikali za mitaa kuboresha uwekezaji katika uzalishaji na utoaji wa huduma kulingana na mahitaji ya jamii;

- Hatua za kuandaa Programu ya Luendeleza Sekta ya Kilimo umeshirikisha wadau mbalimbali kwa mfano serikali, wafadhili, sekta binafsi na taasisi zisizo za kiserikali katika ngazi mbalimbali;

- Mfuko huo unaundwa kama njia ya kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo na kupewa umuhimu katika Mtazamo Mpana wa Sekta kama ilivyokubalika na wadau wa sekta kwa kuzingatia haja ya kuoanisha taratibu za programu ya ASDP na zile za Programu ya Kurekebisha Serikali za Mitaa na Huduma za Umma; na

- Kwa jumla, utekelezaji wa Programu utaimarisha mifumo ya serikali na kupunguza gharama za uendeshaji ili kuwezesha mipango ya wilaya na kitaifa kutekelezwa na wadau kwa ufanisi zaidi.




Mchoro: Mtiririko wa Fedha za Mfuko

Jarida hili sasa linapatikana kwenye mtandao http://www.asdp.go.tz

# Kuendeleza Kilimo kwa Kuzingatia Mtazamo Mpana wa Sekta

## Utangulizi

Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo unatambua maeneo makuu matano ya kimkakati katika kufanikisha kukua kwa sekta na kuondoa umaskini. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ni programu ya utekelezaji wa mkakati huo na inaelekeza jinsi mkakati unavyoweza kutekelezwa kwa kutumia Mtazamo Mpana wa Sekta. Hii imeleta changamoto kwa wadau kuuelewa na kuukubali mtazamo huo na kuweka mifumo stahili ya kuutekeleza. Uelewa finyu wa Mtazamo Mpana wa Sekta umesababisha matatizo katika kutafsiri malengo ya mkakati katika programu thabiti ya kuendeleza sekta.

Utaritibu unaandaliwa ili kuharakisha utekelezaji wa ASDP kwa kutoa maelezo ya kina juu ya vigezo vya maendeleo ili kuwawezesha wadau kuelewa mtazamo mpana wa sekta ni nini na jinsi ya kutathimini utekelezaji wake.

## Mtazamo Mpana wa Sekta ni Nini?

Katika mazingira ya Tanzania, Mtazamo Mpana wa Sekta:

*“ Ni utaratibu wa kufanya kazi kwa pamoja kati ya serikali, wafadhili na sekta binafsi na kupanua umiliki wa serikali katika maamuzi ya sera na uwekezaji katika sekta,kuongeza mahusiano kati ya sera , matumizi ya rasilimali utekelezaji na matokeo na kupunguza gharama za uendeshaji. Unahusisha kuandaa sera na mikakati inayowezesha kuwa na mfumo wa pamoja wa matumizi ya rasilimali za kutoka ndani na nje. Pia kuwa na utaratibu sawia wa kupanga ’kuendesha na kutoa taarifa za utekelezaji wa mipango.*

### Faida na Sababu za Kuzingatia Mtazamo Mpana

- Uandaaji na utekelezaji programu za sekta kwa utaratibu wa SWAp umeonyesha kasi na rahisi zaidi kwa wizara moja kwa mazingira ya Tanzania ambako kuna wizara nyingi zinazohusika na maendeleo ya sekta, utumiaji wa Mtazamo Mpana wa Sekta unatoa changamoto kwa Wizara kuu za Sekta ya Kilimo katika kuyakabili masuala ya jumla ya sekta kwa pamoja;
- Mtazamo Mpana wa Sekta inalenga katika kujumuisha majukumu ya kitaasisi katika kuondoa umaskini kwa kuchangia katika utekelezaji wa MKUKUTA;
- Unaruhusu serikali kutekeleza sera na mipango yake ya kuendeleza sekta kulingana na vipaumbele vyake;
- Unawaruhusu wafadhili kuweka pamoja rasilimali za misaada na mikopo, mawazo, fikra na ushawishi, na kufanya kazi na serikali ili kutatua matatizo ya maendeleo kwa pamoja;
- Unapunguza uwezekano wa kuwa na miradi iliyojitenga nje ya mfumo wa serikali na mingine inayotekelezwa sambamba na mfumo wa serikali; na
- Hurahisisha kuhusisha sekta binafsi katika uendelezaji wa sekta ya kilimo.

Mtazamo Mpana wa Sekta unazitaka Wizara za Sekta ya kilimo kwa ujumla wao kutoa kipaumbele katika kukabiliana na masuala ya sekta, na yale yasiyo yao moja kwa moja lakini utekelezaji wake unachangia maendeleo ya sekta ya kilimo.

## Vipengele vya Mtazamo Mpana wa Sekta

Kuna vipengele saba (angalia mchoro) vinavyohusiana na Mtazamo mpana huo. Sera na mkakati wa sekta ni msingi mkuu wa mtazamo, ikifuatiwa na mfumo thabiti wa matumizi ya rasilimali. Hata hivyo, vyote vilivyoonyeshwa ni muhimu ingawaje baadhi vitaendelea kuimarika kwa kasi tofauti jinsi programu itakavyoendelea kutekelezwa.

Baada ya mtazamo mpana wa sekta kukubalika, programu ya sekta ambayo ni dhahiri/hakika, yenye muda maalum na gharama za utekelezaji inaweza kuandaliwa kulingana na mkakati wa sekta. Kwa hiyo programu huwa inafuata misingi ya mkakati wa sekta uliokubalika ikiwa ni pamoja na mfumo wa matumizi unaoonyesha gharama za muda wa kati, na lazima uwe ni mfumo na mchakato unaoongozwa na serikali ili kuhakiki uratibu wa wafadhili. Mfumo wa sasa wa mfuko wa pamoja wa kugharamia programu ni moja ya hatua ya kuelekea kwenye programu ya ki-sekta.






Wadau (wakurugenzi wa sekta, sekta binafsi na wafadhili) wakiwa kwenye kikao cha kupanga mipango na mikakati ya kutumia mtazamo mpana wa sekta ya kilimo

### Matatizo Yawezayo Kuathiri Kukubalika kwa Mtazamo Mpana wa Sekta

- Wafadhili wengi huongozwa na sera, wajibu na taratibu za nchi zao na mara nyingi si wepesi kuzibadilisha kufuata zile za nchi wanazozifadhili;
- Sekta ya kilimo kimsingi ni shughuli ya sekta binafsi, na mara nyingi kunakuwa na utatanishi wa jinsi gani fedha za umma zitumike ili kugharamia na kuendeleza sekta binafsi;
- Hapa Tanzania, kuna wizara tatu zinazohusika na kuendeleza sekta hii, na kila moja huvutwa na kutaka kutoa kipaumbele kwenye maeneo ambako inawajibika kuliko kuangalia kwa upana zaidi ki-sekta;
- Mtazamo Mpana wa Sekta hutaka watumishi wa serikali wawe waelewa wa matatizo yanayokabili maendeleo ya sekta pamoja na kuelewa vema malengo ya sekta, na pia taratibu mbalimbali za mipango, bajeti na ufuatiliaji;
- Programu ya Kurekebisha Serikali za Mitaa imebadilisha wajibu na madaraka ya watumishi wa wizara kuu za sekta ya kilimo, na jinsi wanavyowezesha maendeleo ya sekta; mabadiliko haya bado hayajajikita sawasawa; na
- Kuingia kwenye Mtazamo Mpana wa Sekta kunategemea wafadhili kuelewa na kukubali kiwango cha uwajibikaji katika mfumo wa umma wa uendeshaji maswala ya fedha.

# Mradi wa Uwekezaji Katika Sekta ya Kilimo Wilayani

## Utangulizi

Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani uko chini ya programu ndogo (A) ya Programu ya Kuenbdeleza Sekta ya Kilimo inayoangalia uwezeshaji na utekelezaji wa sekta ya kilimo wilayani, na ngazi za kata na vijijini. Mradi una lengo la kuongeza uzalishaji na mapato kwa kaya za vijijini ili kuziwezesha kuwa na usalama wa chakula na kuboresha hali zao za maisha kwa wakulima wapatao milioni 3.4 wanaoishi katika eneo la mradi.

Mradi unatarajia kuweka misingi thabiti ya uibuaji, uandaaji na utekelezaji wa Mipango makini wa Kuendeleza Kilimo Vijijini kwa njia ya kuviwezesha na kuvijengea uwezo idadi kubwa ya vikundi na mitandao shiriki ya wakulima; kujenga uwezo wa serikali za mitaa katika uwezeshaji, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya uendelezaji kilimo vijijini na wilayani.

## Maelezo Mafupi Juu ya Mradi

Mradi una maeneo makuu matatu ya utekelezaji wilayani na moja ni la usimamizi wa mradi, na yafuatayo ndiyo matarajio ya kila lengo:

### *Kuwajengea Uwezo Wakulima*

- Wilaya 25 zitakuwa na watendaji wenye uwezo wa kuhamasisha na kufundisha vikundi shirikishi vya wakulima kupitia elimu shirikishi ya watu wazima;



Ushiriki wa wadau ni muhimu sana kwa DASIP

- Wakulima 250,000 kutoka vikundi shirikishi 10,000 vya wakulima watafunzwa teknolojia bora, uongozi bora na ujasiriamali.

### *Mipango na Uwekezaji Katika Kilimo*

- Wilaya 25 zitawezeshwa kuibua, kupanga, na kuendesha Mipango ya Kuendeleza Kilimo;
- Mipango 25 ya Kuendeleza Kilimo Wilayani itaandaliwa na kutekelezwa;
- Mipango 750 ya Kuendeleza Kilimo Vijijini itaandaliwa na kutekelezwa ikijumuisha miradi midogo midogo ya kilimo, miundo mbinu midogo midogo na uwekezaji kwenye kuboresha teknolojia za kilimo;
- Uwezeshaji wa kufikia masoko kupitia matengenezo ya Kilometa 500 za barabara yatakayofanywa na mradi; na
- Uboreshaji wa matumizi ya maji katika kilimo kwa kujenga miundo mbinu 25 ya uvunaji maji.

### *Msaada katika Mitaji na Masoko*

- Uundaji wa vyama endelevu 200 vya Kuweka na Kukopa, kila kimoja kikiwa na zaidi ya wanachama 1,000 na akiba ya shilingi milioni 40 baada ya miaka sita ya uendeshaji; na
- Uundaji na uendeshaji wa masoko ya kilimo kupitia mtandao katika wilaya 25.

### *Uratibu na Uendeshaji Mradi*

- Kitengo cha Uratibu kimeundwa ili kuratibu utekelezaji katika wilaya na taasisi za kiwakala zinazotumika.

## Eneo la Mradi

Mradi utatekelezwa katika wilaya 25 za Biharamulo, Bukoba, Karagwe, Muleba na Ngara (mkoa wa Kagera); Kasulu, Kibondo na Kigoma Vijijini (mkoa wa Kigoma); Bunda, Musoma Vijijini, Tarime na Serengeti (mkoa wa Mara); Geita, Kwimba, Magu, Misungwi, Sengerema na Ukerewe (mkoa wa Mwanza); na Bariadi, Bukombe, Kahama, Kishapu, Maswa, Meatu na Shinyanga Vijijini (mkoa wa Shinyanga).

## Utekelezaji wa Mradi

Mradi utatekelezwa kwa miaka sita kwa kuzingatia muundo wa kitaasisi uliopo wa ASDP.

Karibu shughuli zote za mradi ni za kijamii na zitatokana na mipango ya maendeleo iliyoibuliwa na kupangwa kwa kushirikisha wadau. Timu ya Uendeshaji ya Wilaya ndiyo itakayowajibika katika kuratibu shughuli zote za mradi, na pia katika kuhakiki na kuidhinisha miradi ya kitaalamu kutoka kwa jamii ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji. Uidhinishaji wa miradi ili kupata fedha za utekelezaji utafuata taratibu za utawala rasmi wa wilaya kuanzia baraza la kijiji hadi baraza kuu la wilaya.

## Hali Iliyopo

Mradi huu ambao ofisi yake kuu ya utekelezaji itakuwa katika Jiji la Mwanza, utazinduliwa rasmi katikati mwa Januari, 2006.



Uboreshaji kilimo unahitaji uwekezaji katika mashine na mitambo ya kisasa

Kitengo cha uratibu wa mradi kimeundwa na utaratibu wa kupokea fedha na kuzipeleka wilayani/maeneo ya utekelezaji umekamilika. Pia Kamati ya kitaaluma ya mradi imekwishaundwa.

Shughuli ya kwanza ya mradi itakuwa ya kujenga uwezo wa wadau katika kutekeleza mradi. Uwezeshaji wakulima utahusisha kutoa mafunzo kwa wagani, wakulima na kuhakikisha masuala ya jinsia yanazingatiwa kwa makini. Shughuli hizi zitaanza kwa wakati mmoja mwanzoni mwa mwaka 2006 katika wilaya zote za mradi.

## Tamati

Mradi huu ni shirikishi kwa muundo, madaraka na maamuzi katika utekelezaji yanafanywa na wadau kwa kiasi kikubwa ili kuweka mazingira ya kuwa uendelevu. Mradi unajaribu kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwenye utekelezaji wa Programu Maalum ya Usalama wa Chakula Tanzania uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

# Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani: Mtazamo wa Jumla

## Dhana ya Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani

Serikali imeunda Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo, ambao unatoa mfumo na mwelekeo wa kufikia malengo ya sekta. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, programu iliyoandaliwa na Wizara Kuu za Sekta ya Kilimo hutoa mfumo kamili na mchakato wa utekelezaji wa mkakati wa kuendeleza sekta. Shughuli za maendeleo vijijini zitatekelezwa na mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia mchakato wa mipango ya kuendeleza kilimo wilayani.

Hivi sasa, huduma za ugani na uwekezaji katika kilimo kwenye ngazi ya wilaya hazina mpangilio mzuri wa pamoja na hivyo kutowafikia walengwa kwa utaratibu stahili unaohakikisha uthabiti wa uwajibikaji wa watoa huduma. Kama ilivyoainishwa kwenye ASDP, kumejitokeza ulazima wa wafadhili kufanya kazi kwa karibu na serikali katika kugharamia uwekezaji na kutoa huduma ili kuwezesha utekelezaji wa mipango hiyo kupitia mfuko wa pamoja wa kugharamia Programu unaoundwa kwa mchango wa serikali na wafadhili.

## Mwanzo wa Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani

Chini ya uongozi wa Sekretariati ya Programu, timu ya wataalamu iliundwa Novemba 2004, na kufanya mashauriano na wadau wa sekta. Taarifa yake ilitoa mapendekezo kwamba kuundwe chombo cha serikali na wafadhili cha kusimamia michango ya kuwezesha kuendeleza uwekezaji na utoaji huduma wilayani kwa kuzingatia sera za serikali za utoaji madaraka katika Serikali za Mitaa.



Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani lazima ianzie Vijijini

Umuhimu uliwekwa ili kuhakikisha uandaaji wa mipango hiyo unazingatia ukuaji wa sekta binafsi, na kuwezesha utoaji fedha kwa ajili ya mipango hiyo moja kwa moja kutoka hazina ya serikali. Mipango ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo inatilia maanani malengo ya Programu ya Utoaji Huduma ya Kilimo na utekelezaji wake vijijini.

## Malengo

Programu inalenga katika kuwezesha Serikali za Mitaa kuhimili nafasi zao za utekelezaji na usimamizi ili kufikia malengo ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ya kuboresha na kuongeza faida, tija, na mapato katika kilimo endelevu. Inalenga katika kuwawezesha wakulima kupata na kutumia elimu na teknolojia mpya za kilimo, miundombinu bora na rasilimali; pamoja na kuziwezesha Serikali za Mitaa kupanga, kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma na uwekezaji.

## Utekelezaji

Mfumo wa utekelezaji unajumuisha sekta ya umma na binafsi ambapo wajibu na madaraka ya kutekeleza Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani yako chini ya Sekta ya Umma inayojumuisha Wizara kuu za sekta ya kilimo, wizara zingine, Sekretariati za mikoa, Serikali za Mitaa, kata, mabaraza ya vijiji, bodi za mazao/mifugo; na Sekta Binafsi inajumuisha wazalishaji wa mazao na mifugo, wasindikaji na vikundi vinavyojihusisha na kilimo, taasisi za fedha, taasisi zisizo za kiserikali, taasisi za kijamii na taasisi zisizo za umma.

## Hatua za Uboreshaji

Miongozo juu ya uandaaji, utekelezaji na usimamiaji wa Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani umetayarishwa ili kuongoza mipango ya miaka mitatu ya shughuli zilizopewa vipaumbele na wilaya na shughuli nyingine za sekta ya kilimo, kama sehemu ya Mipango ya Maendeleo ya wilaya

Miongozo inaelezea kwa kina mchakato mzima wa uandaaji wa mpango kwa kutumia mpango shirikishi 'chini-juu' na pia kwa kuzingatia mkakati wa mipango ya wilaya. Inaimarisha uongozi makini kwa wilaya zote katika kuandaa Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani iliyokubuhu na kuhakikisha utekelezaji makini, uwazi na uwajibikaji. Mafunzo juu ya utumiaji wa miongozo yatatolewa kwa wadau katika ngazi zote mwanzoni mwa mwaka 2006.

# Kamati Maalum II ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Yazinduliwa

Kufuatia mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa ya mapitio ya mchakato wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo uliofanyika 2004/2005, Serikali imeafiki kuwa na Kamati Maalum mbili kwa ajili ya mchakato wa uundaji wa Programu hiyo badala ya nne za awali. Hii inalenga kuboresha utendaji na utekelezaji katika kushauri na kusaidia katika kutoa huduma za kitaalamu/sera kwa Kurugenzi za Mipango na Sera za Wizara kuu za sekta ya kilimo katika uwezeshaji wa ushiriki wa wadau, hususan wa sekta binafsi katika kufikia malengo ya Programu hiyo.

Kamati Maalum II ya ASDP ambayo lengo lake kuu ni kufuatilia kufikiwa kwa malengo ya kitaifa ya kuendeleza sera za sekta ya kilimo katika ngazi za serikali za mitaa na sekta binafsi, pamoja na kuibua ari za maendeleo katika maeneo nje ya sekta, ilizinduliwa rasmi katika warsha ya wadau ya tarehe 20 Desemba 2005. Kamati hii iliunda Hadidu za Rejea, na kuthibitisha wanakamati wapatao kumi na sita ambao wanawakilisha sekta ya umma na binafsi pamoja na wafadhili.

**Sekretariati—ASDP, Wizara ya Kilimo na Chakula**
**S.L.P. 9192 Dar es Salaam, TANZANIA**
**Simu: 255-22-286 1344; Faksi: 255-22-286 1344**
**Barua Pepe: asdp@cats-net.com; Tovuti: http://www.asdp.go.tz**

**Sekretariati ya ASDP Inawatakia Mwaka wa Mafanikio wa 2006**